KILOMBERO SUGAR COMPANY

Tarehe 20 Agosti 2025

# SERA YA USALAMA, AFYA, MAZINGIRA, MAJANGA, UBORA WA BIDHAA NA ULINZI.

## 1 UTANGULIZI

1.1 Sera hii inatumika kwa Kampuni ya Sukari Kilombero inayotengeneza Sukari kwa matumizi ya binadamu kutoka kwenye miwa kama malighafi na Illovo Distilleries Tanzania wazalishaji wa Extra Neutral Alcohol (ENA) inayotumia molases kama malighafi. Kuna viwanda viwili vya sukari ambavyo ni kiwanda cha Ruembe (K2) kilichopo wilayani Kilosa na Msolwa (K1) kilichopo wilayani Kilombero vyote viko mkoani Morogoro na kiwanda cha bidhaa za mkondo wa chini ambacho ni Illovo Distilleries Tanzania kilichopo karibu na kiwanda cha sukari Ruembe (K2).

1.2 Sera hii inaelekeza wajibu wa kampuni ya sukari ya Kilombero inayojumuisha viwanda vyake vyote vya sukari na bidhaa za viwanda vya mkondo wa chini kufanikisha mfano bora katika mafanikio ya viwango vya usalama, afya, mazingira, ubora, viwango vya ulinzi na utendaji katika usalama wa chakula.

1.3 Kampuni inajitahidi kuendesha shughuli zake katika dhana ya uwajibikaji, utaalamu na kwa uwezo wa hali ya juu na inaendelea kuweka na kuboresha uendeshaji kuelekea kutimiza lengo kuu la kutokuwa na matukio, ajali, kutofikia malengo, malalamiko au mapungufu yakiubora kwa kiwango kikubwa cha mafanikio.

1.4 Kama kampuni inayoongoza Tanzania kwa uwezo wa uzalishaji wa sukari na bidhaa za mkondo wa chini, Kampuni inatambua wajibu wake kwa wadau wake kwa kupunguza athari za kiafya, usalama, mazingira, ulinzi pamoja na usalama wa chakula zinazohusiana na shughuli zake za uzalishaji na bidhaa, huku inaongeza thamani ya wadau.

1.5 Kampuni inazingatia ubora na usalama wa bidhaa, watu, ulinzi na utunzaji wa mazingira na afya ya wafanyakazi wake na jamii ambako inafanyia shughuli zake kama sehemeu muhimu ya mchakato mzima wa biashara na mikakati ya kiutendaji.

## 2 UWAJIBIKAJI

Katika kutekeleza malengo yake ya uendeshaji wa biashara kwa kuzingatia na kuheshimu watu na mazingira na kuendeleza mifumo bora ya ubora, usalama wa chakula, usalama wa watu, afya, mazingira na ulinzi, Kampuni inaongozwa kwa kanuni zifuatazo:

2.1 ***Uendeshaji bila Madhara***

Kuhamasisha utamaduni wa “uendeshaji bila madhara” ili kulinda, kwa kadri inavyowezekana, afya, usalama na ustawi wa watu wetu, jamii zinazotuzunguka na mazingira katika nchi tunazoendeshea shughuli zetu.

2.2 ***Utunzaji wa Mazingira***

Kutunza kwa ufanisi viumbe hai, mazingira nyeti, matumizi ya ardhi na kutibu maeneo ili kulinda mazingira.

2.3 ***Kupunguza Athari***

Kupunguza athari za biashara yetu kwenye mazingira, kuhamasisha muendelezo na utekelezaji wa tekinolojia isiyoathiri mazingira ili kuhakikisha utunzaji endelevu wa mali asili pamoja na kuweka na kufikia malengo yanayohusiana na ufanisi wa matumizi ya maliasili, upunguzaji wa takataka na kudhibiti uchafuzi wa mazingira

2.4 ***Kuzuia***

Kuzuia matukio makubwa mabaya katika uendeshaji wetu kupitia mfumo wa usimamizi wa majanga wa NOSA, na endapo matukio kama hayo yatatokea, itifaki yenye majibu hufanyika kwa ufanisi ili kupunguza athari na kujirudia.

2.5 ***Kukidhi vigezo***

Kuendesha shughuli zake kwa kuzingatia kanuni na taratibu zilizopo za kiusalama, afya, mazingira, ubora pamoja na ubora wa chakula za ndani na za kimataifa.

Kujitahidi kutekeleza utendaji bora wa viwandani kupitia usimamizi endelevu jumuishi wa majanga wa mfumo wa NOSA, ukiongozwa na kanuni na taratibu za utendaji bora zinazotambulika kimataifa.

2.6 ***Kuheshimu Haki za Binadamu***

Kutoa/kuwezesha mazingira ya kazi yenye misingi inayozingatia kanuni za kuheshimu, mahusiano mazuri ya kazi na mazingira bora ya kazi kwa wafanyakazi wetu sambamba na mikataba, kanuni na taratibu za utendaji bora zinazotambulika kimataifa, na dhamira iliyowekwa kwenye kanuni zetu za maadili na maadili ya kibiashara, na kuwataka wauzaji, makandarasi, watoa huduma na wawakilishi pamoja na watu wengine wanaofanya kazi na Kilombero, kufanya vivyohivyo.

2.7 ***Mafunzo na stadi endelevu***

Kuwezesha uendelezaji wa stadi na ufanisi wa mfanyakazi katika ngazi zote za kampuni, katika kulenga utaratibu wa uzalishaji bora, usalama wa chakula pamoja na ufanisi katika kutekeleza ubora, usalama wa chakula,usalama wa watu,afya,mazingira,majanga na ulinzi.

2.8 ***Ubora***

Kuuza bidhaa salama, zenye ubora na zisizokuwa na viungo au kasoro zinazoweza kuleta madhara au kutishia uhai na afya ya watu, zinazofaa kwa matumizi yaliyokusudiwa, kwa kukidhi sheria za usalama, afya, mazingira, ubora pamoja na usalama wa chakula na viwango vya utendaji bora wa viwanda, na zenye nembo sahihi na kuzitangaza.

2.9 ***Kuhamasisha matumizi sahihi ya bidhaa zetu***

Kuhamasisha wateja na watumiaji wetu kutumia bidhaa zetu ipasavyo na kushiriki malengo yetu ya kiutendaji ya ubora, usalama wa chakula,usalama wa watu,afya,mazingira na ulinzi.

2.10 ***Uboreshaji endelevu***

Kuendeleza na kukuza uelewa wa ubora, usalama wa chakula,usalama wa watu, afya, mazingira na ulinzi. Usimamizi wa hali ya juu wa rasilimali na uwazi katika kutoa taarifa za utendaji ili kufikia dhana ya uboreshaji endelevu katika utendaji kazi, bidhaa, huduma na kuwaridhisha wateja.

2.11 ***Ufanisi katika Mawasiliano na Utoaji wa taarifa***

Mawasiliano na utoaji wa taarifa za kiutendaji za ubora, usalama wa chakula,usalama wa watu,afya,mazingira na ulinzi kwa wadau wa ndani na nje, angalau mara moja kwa mwaka kwa uwazi.

2.12 ***Usimamizi wa Ugavi***

Kushirikiana na wauzaji, watoa huduma, makandarasi na wateja ambao wako tayari kuendesha shughuli zao kwa kuzingatia kanuni na taratibu za utendaji bora ubora, usalama wa chakula,usalama wa watu,afya,mazingira na ulinzi zinazotambulika kimataifa, na kuhamasisha maendeleo endelevu.

2.13 ***Uhusishwaji Wadau***

Kuhamasisha mahusiano mazuri katika maeneo ambayo tunaendesha shughuli zetu kupitia mahusiano yenye tija katika jamii inayotuzunguka, serikali na mamlaka yao, kwa kusudi la kuwa mshiriki hai katika mwendelezo wa kuwezesha ustawi wa kiuchumi na kijamii kwa wadau wetu na kuimarisha uwezo, ikiwa ni pamoja na kuheshimu mila na urithi wa watu.

## 3 UTEKELEZAJI NA UFUATILIAJI

3.1 Sera hii imepitishwa na Mkurugenzi Mtendaji wa nchi/Tanzania - Kampuni ya Sukari ya Kilombero.

3.2 Malengo na taratibu zote zinazohusiana na sera hii zitapitiwa kila mwaka ili kuhakikisha uboreshaji endelevu, utii wa sheria, na ufanisi wa utekelezaji kupitia Usimamizi wa Kudhibiti Hatari za Biashara.

Guy Williams

Mkurugenzi Mtendaji Tanzania.

20th Agosti 2025

Hakiki inayofuata Agosti 2026